Jina: ……..…Nambari Yako: …….……...
102/2
KISWAHILI **Sahihi Yako: ……..……..**
LUGHA
KARATASI YA PILI **Tarehe: ……..……...**
JULAI 2018
MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA PAMOJA KIDATO CHA NNE – 2018

102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
Lugha
JULAI 2018
Saa 2½

MAAGIZO:

Jibu maswali yote.
Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	**80**	

*Karatasi hii ina kurasa **7** zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.*

1. UFAHAMU

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yafuatayo

Tsunami, tetemeko la ardhi baharini iliyotokea Desemba mwaka wa 2004 katika bara la Asia ilikuwa na athari kubwa sana.Watu wasiopungua 170,000 walipoteza maisha yao kutokana na mawimbi yaliyotifuliwa na tsunami hiyo katika Bahari ya Hindi.Madhara ya maafa hayo yalitanda hadi maeneo ya mbali kama upwa wa Afrika Mashariki ulio na umbali wa takriban kilomita 7,000 kutoka kitovu kikuu cha tsunami hiyo. Janga hilil limeibua mjadala kuhusu madhara yanayotokanana nguvu za kimaumbile. Nguvu za kimaumbile zina uwezowa kuzua majanga yasioweza kutarajiwa.Mlima wa volkeno uliotulia unaweza kuvuvumuka na kutapakaza zaha ambayo inaweza kuua maelfu ya watu kama ilivyotokea huko nchini Kongo,

Majanga ya kimaumbile huweza kusababisha maafa,misiba na tanzia isiyokuwa na mshabaha, sio rahisi kuweza kutawasiri akilini kiwango cha madhara ya majanga haya hadi yanapotokea. Baadhi ya majanga ya kimaumbile nia kama vimbunga vya vumbi,zilizazla,mafuriko,tufani, radi,ukame na hata moto.

Licha ya kuwa binadamu hana uwezo wa kuzuia kutokea kwake, zipo hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa. Kwa mfano, yapo maeneo ambapo kutokana na historia ni rahisi kujua nia majanga yepi ambayo huweza kutokea. Kuna maeneno amabapo mafuriko jutokea kila zinaponyesha mvua za mvuo. Jamii inayojikuta katika mazingira hayo inapaswa kujua ni hatua zipi za kuchuua. Mathalan ujenzi wa matuta, kuhimiza wakazi kusakini katika maeneo ya juu ya huduma za dharura za kupambana na maradhi yanayochimbukana na ungi wa maji na kadhalika. Vivyo hivyo na ukame. Ni muhali huweza kujua ukame unatyokea lini. Hata hivyo jamii inaweza kuchukua hatua Fulani ambazo zinachangia kwenye ukame kama ukataji wa miti kiholela Uchimbajiwa chemichemi ni njia nyingine inayoweza kutumiwa hasa kuhakikisha kuwa ikiwa ukame utatokea,watu hawataathirika kutokana na kuyakosa maji ya kutumia.

Wataalamu wameafikiana sasa kuwa baada ya tsunami iliyotokea lazima uwepo mfumo madhubuti wa kuweza kuudodosa mtikisiko wa ardi ambao hutokea muda kabla ya tetemeko lenyewe. Kwa njia hii watu wataweza kuonywa mapema na labda hasara iliyotokea kupunguzwa.

Maswali

a) Ni nini chanzo cha tsunami? (al. 2)

……

……

b) Eleza tokeo kuu la tsunami (al. 2)

……

……

c) Eleza hatua anazochukua binadamu kupambana na majangan ya kimaumbile (al.3)

……

……

……

d) Mbali na majanga ya kimaumbile yaliyotajwa katika makala taja mengine mawili (al.2)

……

……

e) Taja methali inayoweza kufumbata ujumbe wa kifungi hiki. (al.3)

……

……

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu hiki (al. 4)

i) Kuvuvumka

……

ii) Kutwasiri akilini

……

iii) Mvua za mvuo

……

iv) Ungi wa maji.

……

2. Swali la pili muhtasari

Soma kifungu hiki

DHULUMA ZA ZAMANI ZITATULIWE INAVYOSTAHILI

Tume ya ukweli, haki na maridhiano(TJRC) hatimaye imetoa ripoti kuhusu dhuluma zilizotekelezwa miaka ya nyuma kwa Wakenya ambao hadi sasa wanataka waliohusika kuchukuliwa hatua. Ni muhimu kwa kweli kuona haki ikitekelezwa katika taifa hili kwanni linazingatia utawala wa sheria. Baadhi ya dhuluma

Hizo ni mauaji ya Wakenya maarufu katika jamii maarufu kama Gama Pinto, J.M. Kariuki, Kung'u Karumba, Dk Muthiora, Tom Mboya, Prof. Mbai, Titus Adungosi na Robert Ouko.
Vifo hivi vilitokea katika hali ya kutatanisha na ingekuwa vyema kama waliohusika wangechukuliwa sheria.

Kunao wale walioteseka katika vyumba vya chini kwa chini vya Nyayo House, waliofungwa kwa miaka mingi bila sababu, wengine kushuhudia biashara zao zikiangamizwa na serikali na kadhalika. Dhuluma nyingine ni ufisadi, unyakuzi wa ardhi ya taifa yaliyowaacha Wakenya wengi maskwota. Dhuluma hizi, kwa miaka mingi hazijawai kuelezwa kikamilifu ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale waliohusika. Ingawa kila baada ya dhuluma kufanyika tume iliundwa ili kuichunguza, matokeo yake yaliwekwa katika mashumbaka ya ofisi za waliokuwa mamlakani na kimya kikuu kufuatia.

Viongozi hao wa awali, marehemu Jomo Kenyatta, Rais Mstaafu Daniel Moi na mwenzake Mwai Kibaki walizifumbia jicho dhuluma hizo zilipotendeka na pia ripoti zake zilipotolewa. Kinachotuudhi kama Wakenya ni kwamba walijua fika kuwa tume hizo zilitumia pesa nyingi za walipa kodi kushughulikia hasara Fulani iliyokwisha toke kisha inaishia kuwa hasara juu ya hasara maana matokeo yake yaliwekwa kando na kutuwacha na mioyo mizito iliyojaa uchhungu. Serikali ya Jubilee ni ya kwanza kujitolea ilio kushughulikia ripoti za tume hizi. Kwa hakika tunaipongeza kwani ina maana kwamba inataka kuona haki ikitendeka kwa kila mmoja wetu. Lakini endapo maswala haya yatashughulikiwa bila mpango kabambe kuna hatari ya kujiweka nchi hii hatarini.

Sharti mikakati kabame iandaliwqwe ili kazi yenyewe ifanywe bila kufufua machungu ya familia na jamii zilizoguzwa zaidi na dhuluma zenyewe. Ni dhuluma ambazo kwa wengi zimeanza kusahaulika na ninajua sasa zitafufuliwa upya.

Sharti dhuluma hizo kushughulikiwa kwa usawa kwani endapo tutaona dosari zikiibuka katika utekelezaji wa sheria kuhusu dhuluma hizi tutazidi kuumia badala ya kupozwa moyo. Lilio muhimu hapa ni kwamba wale wote waliotajwa katika ripoti kukiri makosa.

a) Fafanua dhuluma zinazorejelewa katika muktadha (maneno 20-30) ***(Al 7)***

……

……

……

……

……

……

b) Dhuluma za zamani zinaweza kutatuliwa vipi (30-40) ***(Al 8)***

……

……

……

……

……

……

3. **<u>MATUMIZI YA LUGHA:</u> (Alama 40)**

(a) Ziandike sentensi zifuatazo ukitumia kiwakilishi cha pekee o-ote. (alama 2)

(i) Ufunguo wowote ufunguao ni wetu.

……

(ii) Ngozi zozote zirarukazo ni za kifaru.

……

(b) Taja sauti zozote ***nne*** zinazotamkiwa katika ufizi. (alama 2)

……

……

(c) Andika sentensi inayoonyesha ‘ki’ ya masharti. (alama 1)

……

(d) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi: Alimkemea. (alama 1)

……

(e) Bainisha matumizi ya ‘ni’ katika senntens zifuatazo. (alama 2)

(i) Ondokeni.

……

(ii) Kiptoo ni mwizi sugu

……

(f) Eleza maana ***nne*** zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

(i) Alimpigia simu

……

……

(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 2)

(i) Vile vingali vikitengenezwa

……

(h) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 3)

(i) Puka chaka hata wewe siamini.

……

(i) Eleza tofauti kati ya sentensi hizi mbili. (alama 2)

(i) Ungesoma kwa bidii ungepasi mtihani.
(ii) Ungalisoma kwa bidii ungalipasi mtihani.

……

……

(j) Andika sentensi moja kwa kutumia ‘licha ya’. (alama 2)

……

……

(k) Andika ukubwa na udogo wa neno rununu. (alama 1)

(i) Ukubwa ……

(ii) Udogo ……

(l) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. (alama 3)

(i) Domo limepinduliwa.

……

(ii) Kiwiko kimejigonga ukutani.

……

(iii) Ukimwi umeangamiza wengi duniani.

……

(m) Unda vivumishi kutokana na maneno yafuatayo. (alama 2)

(i) Imani

……

(ii) Ubora

……

(n) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendesha. (alama 2)

(i) – nya ……

(ii) - cha ……

(o) Taja maana ***mbili*** ya neno ‘mjomba’. (alama 2)

……

……

(p) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Ala! Huna heshima wewe mtoto!”

Mama alimkaripia bintiye:

……

……

(q) Kamilisha methali zifuatazo. (alama 2)

(i) Ukuni juu ya uchaga .....

(ii) Simbiko haisimbuki ila .....

(r) Eleza maana ya misemo ifuatayo. (alama 3)

(i) Msumari wa moto juu ya kidonda.

……

(ii) Pasulia mbarika.

……

(iii) Giza la ukata.

……

(s) Onyesha kirai nomino, kirai kivumishi na kirai kielezi katika sentensi. (alama 3)

(i) Bawabu mzuri huandika ripoti ndefu mara kwa mara.

……

……

4. ISIMU - JAMII

(a) Eleza ukionyesha bayana tofauti baina ya lahaja na lafudhi. (alama 4)

……

……

……

……

(b) Taja sifa tambulizi za lugha ya misimu (alama 3)

……

……

……

(c) Orodhesha sifa kuu za sajili ya siasa. (alama 3)

……

……

……